

# Muungano wa mabadiliko wa uvuvi wa kukokota

## Muungano wa kimataifa wa mabadiliko wa uvuvi wa kukokota

Miaka ya hivi karibuni jumuiya hii imetuonyesha uwezo wake wa kujijenga na uhamasishaji wa raia. Kote ulimwenguni, mamilioni ya watu wameingia barabarani kupinga udhalimu wa rangi na kutokuchukua hatua kwa uharibifu wa mabadiliko ya tabia nchi. Maandalizi ya chini yamepelekea ongezeko la harakati za kimataifa. Tumegundua kuwa kuondoa mfumo huu, masuala mengine sugu, tunahitaji kukutana pamoja kuliko wakati wowote ule.

Ndiyo maana tunataka kuimarisha harakati za ulimwengu kukabiliana na uvuvi haribifu na kurejesha hali nzuri kwenye bahari yetu. Umoja wetu wa wavuvi wadogo unakuwa, Hii ni muungano mpana ya wavuvi wadogo, viwanda vya samaki, wahifadhi, waendeshaji wa ndani wa biashara ya utalii,, wanasayansi, mameneja na wataalam wa sera za uvuvi ambao wamejitolea  kwa pamoja, kuleta mabadiliko yanayohitajika. Sisi tunaunga mkono uvuvi madogo,  tunaunga mkono  mazingira bora na tumedhamiria kuweka mbele mahitaji ya jamii ya mwambao wa pwani

Harakati zetu zitaratibu uvuvi mmoja haribifu zaidi - uvuvi wa kukokota - pamoja na kuundalia sera sahihi na kuwa na sauti ya pamoja.  Tutaandaa sehemu salama ambapo jamii itaweza kuelezea namna gani uvuvi wa kukokota unaathiri hali zao maisha yao na usalama wa chakula, na kuandaa suluhisho zinazowafaa. Tutazishirikiana na meli za wazawa/ndani  kuchunguza njia mbadala na kuwezesha upatikanaji angalau wa njia ya

mpito. Wakati huo huo, kwa pamoja tutazungumzia dhidi ya tasnia ya uvuvi ya viwanda yenye nguvu nyingi za kisiasa kwa njia ambayo ingeleta hatari kubwa kwa watu binafsi. Kwa utaratibu huu  muungano utajitahidi kuwajengea uwezo, kwa uwiano sawa, watu wote ambao kipato chao kinategemea ustawi mzuri wa rasilimali za bahari.

# Wito wetu kwa hatua

## Kushinda dharura ya bahari

Bahari yetu haijawahi kuwa muhimu sana, wala haijawaji kuathiriwa sana. Bahari inatoa mwelekeo wa mabadiliko ya tabia chi na hali ya hewa.  Ndiyo inayotowa hewa ya oksijeni kwa wote na protini kwa watu wengi. Ni makaazii ya  viumbe hai vingi. Hata hivyo inashabuliwa kutoka pande zote. Uvuvi kupita kiasi, uchafuzi wa mazingira, na uharibifu wa hali ya hewa. Maswala haya yanabadilisha bahari kwa njia ambazo hatukuwahi kuziona hapo awali. Yanaharibu  bahari yetu, na kutishia idadi ya samaki ambayo hutoa  chakula kwa mabilioni na chanzo cha vipato  kwa mamia ya mamilioni ya jamii ya mwambao wa pwani.

Lakini wakati tukijua kutatua matatizo hali ya hewa ni magumu sana, kumaliza uvuvi kupita kiasi ni rahisi sana. Tunayajua matatizo na tunajua jinsi ya tatua.  Tunajua yanaweza kutatuliwa kwa kuwepo sera  madhubuti, inayotekelezwa kimataifa. Tunajua kwa kufanya hivyo tutaifanya bahari na vilivyomo kuwa himilivu na ulimwengu wa joto.

Tunaamini kuwa kurekebisha uvuvi kupita kiasi ni moja kati ya muhimu sana tunaloweza kufanya kupunguza hatari za bahari. Na tunaamini kuwa jambo hili linapaswa kuanza kwa kuondoa uvuvi haribifu wa viwanda ambao hufanya kiasi kikubwa cha uharibifu wa bahari.

## Uhitaji wa kukabiliana na uvuvi wa kukokota

Uvuvi wa kokota ni moja kati ya nyenzo maaruufu zinazotumika kwa uvuvi wa viwanda kuvua samaki na moja kati ya mbinu haribifu ya uvunaji wa samaki. Uvuvi wa kukokota

kwa meli kwa nyavu zenye uzito mkubwa kwenye sakafu ya bahari na nyasi, huvua kiasi cha tani milioni 19 za mazao ya bahari kwa mwaka. Kiwango hiki ni robo ya uvunaji wa mazao ya bahari yanayovuliwa kimataifa na ni kiwangu kikubwa kinachovuliwa kuliko zana nyengine yotote duniani. Katika maeneo mengine ya dunia zaidi ya nusu ya mazao yabahari huvuliwa kwa kutumia njia hizi.

Ni matumizi ambayo huharibu bahari zetu na wale wote ambao chakula chao na maisha yao hutegemea bahari. Nyavu za kukokota zenye upana kama uwanja wa mpira hukokora sakafu ya bahari na nyasi, huharibu kiasi kikubwa cha maisha ya viumbe wa bahari. chini ya bahari, na kuharibu idadi kubwa ya viumbe vya baharini. Makazi ya viumbe wa baharini yaliyoharibika ambayo hutoa chakula na kivuli kwa idadi kubwa ya viumbe wa baharini huweza kuvunjwa kwa dakika chache tu. Maengi yao hayawezi kujirejesha.

Uvuvi wa aina huu hauchagui. Marekebisho ya zana za uvuvi na usimamizi bora umeboresha mambo, lakini kwa bahati mbaya viumbe vingi vya baharini bado vinaendelea kuvuvliwa. Katika kipindi cha miaka 65 iliyopita, wavuvi wa kukokota wametupa baharini zaidi ya tani milioni 400 za viumbe wa bahari wasiokusudiwa kuvuliwa. Hii ni pamoja na kila kitu kuanzia kwa aina ya samaki waliohifadhiwa na viumbe wengine wa baharini weneye wenye thamani ya kibiashara nao pia wanalengwa na wavuvi wadogo. Ikiwa samaki hawa wangepelekwa bandarini, wangekuwa na thamani ya karibu dola bilioni 560 za Kimarekani.

Uharibifu uliofanywa na uvuvi wa kukokota ni mkubwa zaidi kuliko ule wa upotezaji wa viumbe hai vya baharini wa kawaida. Zaidi ya watu milioni 100 wanategemea uvuvi wa maji madogo kwa maisha yao ya kila siku- ambao mara nyingi hutumia bahari hiyo hiyo inatoyumiwa na wavuvi wa kukokota. Kwa kuyaharibu makaazi ya samani na kudhoofisha idadi ya samaki, uvuvi wa kukokota huleta migogoro na hupunguza uvuvi ambao ni muhimu kwa maisha na chakula wa watu wengine waliomo katika mazingira magumu zaidi duniani.

## Athari za hali ya hewa

Pia kuna madhara yatokanayo na hali ya hewa. Vipande vya baharini na makazi ya samaki yaliyoharibiwa na nyavu za kukokota ni hifadhi kubwa zaidi ulimwenguni za

hewa kaa. Kila mwaka,uvuvi wa kukokota hutoa wastani wa tani bilioni moja ya $CO_2$ kutoka baharini, kiasi ambacho wengine wamefananisha na uzalishaji kutoka kwa sekta nzima ya ndege za angani. Hata hivyo hakuna uhakika ni kiasi gani ya hewa ukaa hiyo itakaa baharini na ni kiasi gani kitakachoishia angani, kuna uwezekano kuongeza zaidi bahari zetu na kudhoofisha zaidi uzalishaji na bioanuwai. Zaidi ya hayo kuna ongezeko ya hewa ukaa kutokana na shughuli za wavuvi wa kukokota ambayo hutoa hewa ukaa zaidi ya aina nyingine yeyote ya uzalishaji wa chakula. Kuweka kwa urahisi, biashara-kama-kawaida katika harakati za uvuvi wa kukokota haiendani na mikakati ya kimataifa ya kupunguza hewa ukaa kabisa.

## Uvuvi mdogo bora, mazingira bora

Hii ni kusema kuwa, tunatambua kuwa sio wavuvi wote wa kukokota unauharibifu sawa na makaazi ya samaki, idadi ya samaki, na sayari. Kuna wavuvi wachache wa wavuvi wadogo ambao hutumia nyavu za kukokota zinazotumiwa na baharia, makasia na hata mashine. Wao wana mchango mdogo kwenye samaki wanaovuliwa, na sio walengwa wa wito huu.

Tunalenga kuangazia meli zinazotumia mashine za kuvuta nyavu za kukokota wakivua katika maji ya machache na maeneo ya bahari yaliyolindwa ulimwenguni. Uvuvi wa kukokota kama huo, tunaamini, kwa asili ni mkubwa, , kwa asili ni mbaya kwa usalama wa chakula wa muda mrefu, na, pale ambapo kuna mfumo mzuri wa makaazi ya samaki, kwa asili huharibiwa.   Katika sehemu nyingi za dunia, kuna uvuvi wa kukokota ambao huitwa ni "uvuvi mdogo". Kuna uvuvi wa kukokota  Indonesia, Ufilipino, uvuvi mdogo kwenye jumuiya ya Ulaya.. Lakini meli kama hizo ni ndogo kwamajina tu, na hutengenezwa kwa lengo la kuweza kuvua katika maji madogo yaliyotengwa kwa wavuvi wadogo. Kwa ujazo wowote au uwezo, huu ni uvuvi mkubwa, na kwa hiyo yanabadilishwa  kwa makubaliano ya pamoja.

## Mwisho wa ruzuku na haki

Tunatambua kuwa meli nyingi za uvuvi wa kukokota hazijaundwa kwa makusudi ya uharibifu wa mazingira, isipokuwa ni matokeo ya mataifa kutoa mapunguzo kwa uvuvi huu na sheria mbovu. Uvuvi wa kokota hupokea mamia ya mamilioni ya dola katika

ruzuku ya kila mwaka ya ulimwengu, lakini hawalipi chochote kwa uharibifu wanaoufanya wa makaazi, kudhoofisha usalama wa chakula na kusukuma idadi kubwa ya hewa ukaa ($CO_2$) baharini na angani. Ruzuku kama hizo ni mojawapo ya kasoro kubwa ya soko ambayo bahari imewahi kuona, na inaendelea kupendekeza uvuvi ambao kwa njia nyingine hauwezi kudumu kifedha.

Wakati tukitambua kuwa baadhi ya meli hizi za uvuvi zimekuwa na faida ya muda mfupi kwa jamii za pwani (kwa kutoa ajira kwenye meli na vifaa vya uchakataji, na chambo kwa wavuvi wadogo), kwa muda mrefu, kuvua kwa njia hii sio endelevu. Historia inatuambia kuwa masaibu ya kupungua kwa uvuvi yanazidi manufaa ya muda mfupi kwa uvuvi haribifu. Ndio maana tunataka kuona mataifa yakikabiliana na mapungufu yenye madhara na kuchukua hatua zinazofaa kuunga mkono mabadiliko tegemewa.kulinda haki zisizotimizwa za wavuvi na kuondosha madhara ya uzuiaji wa uvuvi wa kukokota yasiyotegemewa.

# Tunatoa wito gani?

Uvuvi wa kukokota ni kesi maalum: inadhoofisha usalama wa chakula kwa jamii na inaleta mgongano kwa jamii nyonge za pwani zilizo. Hakuna njia nyingine ya uvuvi inayosababisha uharibifu mwingi. Hakuna njia nyingine ya uvuvi isiyokubaliana na njia ya sifuri wavu. Kwa sayari, kwa bahari na kwa mamia ya mamilioni ya watu wanaotegemea kwa chakula na riziki, kwa kiasi kikubwa tunahitaji kubadilisha uvuvi wa kokota sasa hivi.

## Tunataka kuona uvuvi wa kokota unaondoshwa kwa haraka na mataifa yote ya mwambao wa pwani, kwa ushahidi wa punguzo la kimataifa la mwaka 2030.

Ili kusaidia kufikia lengo hili, tunayataka Mataifa, kwa mashirikiano na wafanyakazi wa mashirikia ya uvuvi na wadau wengine: wakishauriana na mashirika ya wafanyikazi wa viwanda za samaki na wadau wengine, kuwa:

1. Kuanzisha, kupanua na kuimarisha yaliyotengwa kitaifa (IEZS) kwa wavuvuvi wadogo ambao uvuvi wa meli unakatazwa..

2. Kupiga marufuku uvuvi wa kokota katika maeneo yote tengefu ya bahari (nje ya IEZs) kuhakikisha makazi na mazingira yaliyohatarini kuharibiwa yanalindwa kikamilifu na yanaweza kujirejeshakiwa sawa.

3. Kukomesha mapunguzo ya ruzuku kwa uvuvi wa kukokota na kutenga rasilimali za kifedha na kiufundi kusaidia uondoshaji mzuri wa meli hizi.

4. Kuzuia uongezekaji wa uvuvi wa kukokota kwa maeneo mapya, ambayo hayajavuliwa kwa njia ya kukokota.

Kwa maelezo zaidi, au kuwasiliana nasi, tafadhali tembelea
www.transformbottomtrawling.org